OFISI YA WAZIRI MKUU
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
NYANDA ZA JUU KUSINI SHULE BINAFSI ZA SEKONDARI
MTIHANI WA PAMOJA MUJUMUISHO WA SHULE MBALIMBALI
KIDATO CHA NNE

021 **KISWAHILI**

(Kwa watahiniwa walioko na wasiokuwa shuleni)

MUDA: SAA 3:00 **JULAI, 2026**

Maelekezo

1. Kratasi hii ina sehemu A, B na C zenye jumla ya maswali **kumi na moja (11).**

2. Jibu maswali **yote** katika sehemu **A** na **B** na maswali **mawili (2)** kutoka sehemu C ambapo **swali la tisa (9)** ni lazima.

3. Sehemu A ina alama **kumi na sita (16)**, sehemu B alama **hamsini na nne (54)** na sehemu C ina alama **thelathini (30).**
4. Zingatia maelekezo ya **kila sehemu** na ya **kila swali**.
5. Majibu yote yaandikwe kwa kalamu yenye wino wa **bluu** au **mweusi**.

6. Vifaa vya mawasiliano na vitu visivyoruhusiwa **havitakiwi** katika chumba cha mtihani.

7. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa karatasi zako za kujibia.

S.H.P.S.S KIDATO CHA NNE JULAI, 2026
wazaliwu.com

SEHEMU A (Alama 16)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii

1. Katika kipengele (i) – (x), chagua herufi ya jibu sahihi kisha andika herufi ya jibu kwenye kijisanduku chako cha kujibia.

(i) " Serikali imeweka mikakati kabambe ili kupunguza umaskini ." Neno "**ili**" katika sentensi hii ni aina gani ya neno?

A. Kivumishi C. Kihisishi
B. Kiwakilishi D. Kielezi E. Kiunganishi

(ii) Upi ni mzizi sahihi wa kitenzi "anakula"?

A. Kul C. L
B. La D. Kula E. A

(iii) Mtumiaji wa lugha anapotamka neno kuna sehemu mojawapo katika neno huongeza nguvu katika kutamka kuzidi nyingine, hali hiyo huitwa:-

A. Mkazo C. Uziadadufu
B. Kiimno D. Ukelele E. Msistizo

(iv) Katika mkabala wa kimapokeo au kidhima sentensi yoyote ya Kiswahili huwa na sehemu kuu mbili. Kwa kuzingatia kugezo hiki sehemu hizo ni:- A. Kirai na kishazi tegemezi

B. Kishazi huru na kishazi tegemezi
C. Kirai nomino na kirai kitenzi
D. Kiima na kiarifu
E. Kirai na kishazi

(v) Bainisha tabia ya umbo lililopigiwa mstari katika kitenzi ib-**w**-a

A. Kauli tendeka C. Kauli tendeana
B. Kauli tendea D. Kauli tendwa E. Kauli tendesha

(vi) Zifuatazo ni dhima za picha na michoro katika kamusi isipokuwa ipi?

A. Huvuta umakini kwa watumiaji wa kamusi
B. Huchafua kamusi na kufanya ichukize kwa watumiaji
C. Huwawezesha watumiaji wa kamusi kuunda dhana ya jambo
D. Huwawezesha watumiaji kamusi kuona mfanano E. Maumbo hunata katika kumbukumbu za watumiaji

(vii) Kila asubuhi Maria husimuliwa hadithi na Mwalimu wake wa Kiswahili. Jana asubuhi Mwalimu aliwasimulia umuhimu wa kuwa watoto wema na kumalizia kwa kusema "Mdharau mwiba huota tende" Je unadhani hiyo ililkuwa ni aina gani ya hadithi?

A. Kisasili C. Kisakale
B. Ngano D. Tarihi E. Kigano

S.H.P.S.S KIDATO CHANE JULAI, 2026
wazazihub.com

(viii) Ipi ni fasili sahihi kuhusu ‘vina’ miongoni mwa fasili zifuatazo ;

A. Mstari wa mwisho wa ubeti wa ushairi wenye kujirudiarudia kutoka ubeti mmoja hadi mwingine ;
B. Silabi za mwanzo katika mistari ya beti za shairi
C. Silabi za kati na mwisho za mstari wa ubeti wa shairi zenye mlio unaofanana
D. Kifungu cha maneno kinachobeba wazo kuu mojawapo la ushairi
E. Idadi ya silabi zinazopatikana katika mstari wa ubeti wa ushairi

(ix) Hoja za msingi za mtazamo wa Kiswahili asili yake ni kiarabu umeegemea katika:-

A. Msamiati
B. Msamiati na dini ya kiislamu
C. Msamiati na waarabu kuoa waafrika
D. Dini ya Kiislamu na biashara ya utumwa
E. Msamiati na lugha za kibantu

(x) “Uzuriwe” neno hili limefupishwa katika shairi ili kuleta ulinganifu wa Mizani, ni mbinu ipi imetumika kufupisha neno hilo?

A. Inkisari C.Ufupisho
B. Islafu D. Uhulutishaji E. Tafsida

2. Chagua kifungu cha maneno kutoka **orodha A**, kinachotoa maelezo sahihi ya kifungu cha maneno kutoka katika **orodha B** kisha Andika jibu sahihi katika karatasi ya kujibia.

ORODHA A	**ORODHA B**
i) Sarufi maumbo ii) Sarufi matamshi iii) Sarufi muundo iv) Sarufi maana v) Prediketa vi) Mbuzi aliyechinjwa leo asubuhi	A. Semantiki B. Sintaksia C. Fonolojia D. Mofolojia E. Kikundi kielezi F. Kikundi nomino G. Kikundi kitenzi H. Kishazi tegemezi I. Sentensi changamano

SEHEMU B (Alama 54)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii

3. Hamisi alikuwa haelewi maana ya Silabi na miundo yake , lakini wewe ni mjuzi katika hili. Mfafanulie Hamis maana ya silabi na miundo minne ya silabi kwa mifano tofauti.

4. Eleza maana ya kirai nomino kisha taja miundo minne ya kirai nomino.

S.H.P.S.S KIDATO CHA NNE JULAI, 2026
wazaeli.com

5. a) Nini maana ya kidahizo?
   b) Eleza umuhimu wa kidahizo katika kamusi Toa hoja nne

6. Wajerumani walisaidia sana kukuza na kueneza Kiswahili kupitia shughuli zao. Kwa kiasi Fulani shughuli hizo zilichangia kudumaza Kiswahili. Kwa kutumia hoja nne onesha namna shughuli hizo zilivyochangia kukidumaza Kiswahili.

7. Joka la mdimu ni riwaya inayosawiri maisha halisi ya mwanaume katika jamii. Kwa kumtumia muhusika Amani onesha jinsi gani anavyokubalika katika jamii kama kielelezo chanya cha mwanaume. Toa hoja nne
8. Soma shairi lifuatalo kisha jibu maswali yanayofuata.

   Wa ubani Rawaziri, na kandoro kadhalika,
   Lumbano la kishairi, Gazetini kuliweka,
   Nami nimejikusuri, maoni kuyatamka, Ua
   ni ruwaza njema, tuzo ya mtu kupewa.

   Kutunzwa watu wa enzi, kw aua sijaridhika,
   Siyo Zawadi azizi, hasa inoheshimika,
   Bado hamjamaizi, kwa tunzo inositika, Ua
   ni ruwaza njema, tuzo ya mtu kupewa.

   Ua kupewa harusi, nikaha inapofika,
   Ni siku ya taanusi, kwa bibi kuheshimika,
   Lakini ua si tusi, kwa dume kulipachika,
   Ua ni ruwaza njema, tuzo ya mtu kupewa.

   Ua tuzo ya mahaba, wapenzi wanahusika,
   Ishara ya usuhaba, wawili kukutanika,
   Lakini na makahaba, na wao hujipachika,
   Ua ni ruwaza njema, tuzo ya mtu kupewa.

   Ua likiwa mtini, huwa linanawirika,
   Huwa na kubwa thamani, hapo linapojishika,
   Likitiwa mikononi, si muda linanyauka, Ua ni
   ruwaza njema, tuzo ya mtu kupewa.

   Maswali
   (i) Taja Kichwa cha shairi hili.
   (ii) Ipi dhamira ya mtunzi katika ubeti wa tatu?
   (iii) Taja vina vya kati na mwisho katika ubeti wa kwanza.
   (iv) Mwandishi ametumia aina gani ya mshororo wa mwisho katika beti zake?
   (v) Taja mafunzo mawili yanayopatikana katika shairi hili.

SEHEMU C (Alama 30)

S.H.P.S.SIKIDATO GIMU JUNE JULAI, 2026
wazagimu.com

Jibu maswali **mawili (2)** kutoka sehemu hii, **swali la tisa (9)** ni lazima.

9. “Washairi hutumia miundo mbalimbali katika kupamba kazi yao”. Kwa kutumia diwani mbili ulizosoma onesha miundo mbalimbali iliyotumika katika kusawiri kazi zao. Toa hoja tatu katika kila kitabu

10. “Waandishi wa riwaya wamejadili maadui mbalimbali wanaorudisha nyuma maendeleo ya jamii”. Kwa kutumia riwaya mbili ulizosoma thibitisha kauli hiyo. Toa hoja tatu katika kila kitabu

11. “Pametokea mvutano kuhusu uhusiano kati ya mandhari na mchango wake katika kuibua dhamira”. Tumia tamthiliya mbili kati ya ulizosoma kufafanua uhusiano huo kwa kutoa hoja tatu kwa kila tamthiliya.

S.H.P.S.Ss KIDATO CHA NNE JULAI, 2026
wazaeiimu.com